TARAWEHE

Salatu `t- Tarawih

Kimeandikwa na:
Shaikh Abdul Karim Al Bahbahani

Kimetarjumiwa na:
Ustadh Abdallah Mohamed

Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 - 9987 - 427 - 55 - 0

Kimeandikwa na:
Shaikh Abdul Karim Al Bahbahani

Kimetarjumiwa na:
Ustadh Abdallah Mohamed

Kimehaririwa na:
Sheikh Harun Pingili

Kupangwa katika Kompyuta na:
Ukhti Pili Rajab.

Toleo la kwanza: Februari, 2008
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
P.O. Box 19701
Dar es Salaam, Tanzania
Simu:+255 22 2110640
Simu/Fax: +255 22 2127555
Email: alitrah@raha.com
Website: www.alitrah.org
Online: www.alitrah.info

YALIYOMO

1. Swala ya Tarawehe ni Sunna au Bid'a?.....2

2. Qur'an na Hadithi zakanusha kuweko swala ya Tarawehe.....3

3. Lini imeanza Swala ya Tarawehe?.....4

4. Maoni ya Shia Imamiyya juu ya swala ya Tarawehe.....9

5. Swala ya Tarawehe katika nass za Ahlul Bayt.....10

6. Sunna ya Mtume katika Riwaya za Ahlul-Bait.....12

7. Msimamo wa Sahihi mbili juu ya Swala ya Tarawehe.....14

8. Mjadala kuhusu sahihi mbili.....16

9. Kukusanya watu nyuma ya Imamu mmoja wakati wa Khalifa Umar.....18

10. Kuweka sharia ni jambo maalum kwa Mwenyeezi Mungu.....21

11. Uongo ili kujiepusha na aibu ya bid'a.....24

12. Hitimisho.....31

Neno la mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kwa jina la: "Swalatu'l-Tarawehe" Sisi tumekiita: **"Tarawehe"**

Swala ya Tarawehe ni Swala ya sunna inayoswaliwa mwezi wa Ramadhani na wafuasi wa madhehebu ya Sunni. Madhebu ya Shi'a Ithanaasheri (na Baadhi ya Masunni) hawaiswali Swala hii, na wanasema kwamba ni *bida'a.* Kwa hiyo, kumekuwa na kushutumiana na kutoafikiana baina ya madhehebu hizi mbili juu ya suala hili. Je, upi ni ukweli?

Mwandishi wa kitabu hiki **Shaikh Abdul Karim Al Bahbahani** analijadili suala hili kwa upeo wake kwa kutumia Qur'an, Sunna, na hoja za kielimu pamoja na mantiki, na kumuacha msomaji aamue mwenyewe ukweli ni upi kati ya kuitekeleza Swala ya Tarawehe au kutoitekeleza, au iwapo ni bida'a au sio bida'a.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya **'Al-Itrah Foundation'** imeona ikitoe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, kwa madhumuni yake yale yale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya dini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu: **Ustadh Abdallah Mohamed** kwa kukubali jukumu hili la kukifanyia tarjuma kitabu hiki. Vilevile

tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
S. L. P. 19701
Dar-es-Salaam, Tanzania.

UTANGULIZI

Swala ya Tarawehe, ni Sunna au bid'a?

Wajib, katika sharia ya kiislamu, ni yale yanayomlazimu mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, kuyafanya, kwa kuzingatia kuwa ni mambo ya faradhi ili kufikia ukamilifu utakikanao, kwa kuwa kutokamilisha kutekeleza wajib unaohitajika ni kutofikia daraja inayohitajika.

Na *Mustahabbu* na *Sunna*, ni yale mambo yanayomzidishia ukamilifu na kuwa karibu zaidi na Mwenyezi Mungu (s.w.t.) yule mu'min mwenye kulazimika na kutekeleza wajib.

Swala za faradhi za kila siku ni lazima kwa mtu kuziswali kwa vyovyote itakavyokuwa, lakini kujilazimisha kuziswali mwanzo wa wakati wake kabisa huzingatiwa kuwa ni fadhila na ukamilifu na kuwa muumini huwa anazingatiwa kutilia umuhimu sana faradhi hii ya Mwenyezi Mungu aliyomtukuza nayo Allah; vilevile kuzitekeleza kwa jamaa ni Sunna ambayo pia ni kuhakikisha daraja yake nyingine ya juu ya ukamilifu anaposwali kwa jamaa.

Ibada, katika sharia ya kiislamu zinabainika kwa mambo yafuatayo:
Aina zake na uwezo wake kulingana na nyakati na hali tofauti anazozipitia mwanadamu katika maisha yake yote, na mkusanyiko wake kutokana na nyakati mbalimbali za mwanadamu tokea anapobaleghe mpaka mwisho wa maisha yake., mfululizo huu unaonyesha jinsi gani ulivyo upeo wa Uislamu unavyozingatia sana malezi ya mwanadamu, malezi ambayo hayawezi kuhakikishwa ila kwa kwenda hatua kwa hatua na kuyafanya kwa uzuri na kufungamana na Mwenyezi Mungu (s.w.t.).

Vilevile ibada za kiislamu zinabainika kuwa zimeshapangiwa namna yake, jinsi yake na ufafanuzi wake; mwanadamu hana haki ya kupunguza au

kuzidisha chochote katika hizo kwa rai yake, na juu ya hilo ndio upo muwafaka wa kongamano la waislamu wote.

Kutokana na hali hiyo tunaona kuna umuhimu wa kufanya utafiti kuhusu Swala inayoswaliwa na baadhi ya waislamu katika mwezi wa Ramadhani iitwayo Swala ya Taraweh, je imewekwa na Mwenye kuweka sharia, Mwenye hekima na akabainisha hukmu na ufafanuzi wake? Au haikuwekwa katika sharia ya kiislamu na hivyo kuwa ni bid'a iliyoharamishwa? Ambayo haina msingi katika Qur'ani wala Hadith za Mtume?

* * * * *

Shaikh Abdul Karim Al Bahbahani

Qura'n na Hadith zakanusha kuweko Swala ya Tarawehe

Tunaposoma Kitabu kitukufu hatukuti katika Aya zake athari yeyote ya Swala ya tarawehi, lau kama kungelikuwa na athari ya Qur'an juu ya hiyo, basi mafakihi wa madhehebu manne wangeshikamana nayo, na hatujaona hata mmoja wao aliyetoa dalili juu ya hilo kutoka katika Qur'ani Tsukufu.

Aidha tunaporudi kwenye sera ya Mtume (s.a.w.) pia hatupati upokezi wowote wa Swala ya Tarawehi. Bali tunapata usisitizo juu ya kuswali Swala za usiku katika mwezi wa Ramadhani, lakini kwa kuswali mtu mmoja mmoja na si kwa jamaa.

Na mapokezi yanasisitiza - kama yatakavyokuja - kwamba Swala ya Tarawehe hakuleta Mtume wala haikuwepo wakati wake, bali pia haikuwepo hata wakati wa Abu Bakr, wala pia Mwenyezi Mungu hakuweka watu kukusanyika kwa ajili ya Swala ya Sunna miongoni mwa Sunna zilizopen-

dekezwa, ila Swala ya kuomba mvua tu.

Ila tu ameifanya jamaa kuwa sheria katika Swala za wajib kama vile, faradhi tano za kila siku, Swala ya Tawaf,* na Swala za ayat, na za kumswalia maiti n.k.

Mtume (s.a.w.) alikuwa akisimama usiku wa mwezi wa Ramadhani na akitekeleza Sunna zake bila ya kuswali jamaa na alikuwa akihimiza kuswali Swala hizo na watu wakawa wakifanya kwa jinsi ya walivyomuona yeye (s.a.w.) akifanya.na hivi ndivyo ilivyokuwa wakati wa Abu Bakr mpaka alipondoka mwaka wa kumi na tatu wa Hijiriyya.[1]

Akachukua uongozi baada yake Umar bin Khattab, akafunga mwezi wa Ramadhani wa mwaka huo na hakubadilisha chochote.

Lini imeanza Swala ya Tarawehe?

Ulipofika mwezi wa Ramadhani ya mwaka wa kumi na nne, Umar alikwenda msikitini akiwa na wenzake, akaona watu wanaswali Sunna zao, kuna miongoni mwao waliosimama, kuna waliokaa, waliorukuu, waliosujudu, wasomao na wanaoleta tasbihi, kuna wenye kuhirimia na wengine wenye kuleta takbir na kuna waliokuwa wakitoa salaam; mandhari hayo hayakumpendeza akataka kuyarekebisha kulingana na rai yake, ndipo akawafanyia Sunna tarawehe[2] mwanzoni mwa usiku wa mwezi wa

[1] Hiyo ilikuwa ni usiku wa jumatano ya mwezi nane, Jumadal-Ula na ukhalifa wake ulidumu kwa muda wa miaka miwili, miezi mitatu na siku kumi.

*Wanachuoni wamehoji uhalali wa kuswaliwa salat al-Tawaf kwa jamaa. Hii ni kwa sababu ya ukosefu wa ushahidi wowote kutoka katika hadithi zioneshazo kuwa Mtukufu Mtume (s) aliwahi kuswali swala hii kwa jamaa (Rejea: *Kitab al-Salah* cha Marhum Sayyid al-Khui (r.a.) Jz. 5, Sehemu ya 2 uk. 13.

[2] Hii ni Swala ya jamaa iswaliwayo katika masiku ya mwezi wa Ramadhani, imeitwa *Tarwih* kwa kuwa anayeswali hupumzika kila baada ya rakaa nne.

Ramadhani, akafanya hukmu na akawaandikia miji mingine na akaweka maimamu wawili hapo Madina wa kuwaswalisha watu Tarawehe, mmoja wa wanaume na mmoja wa wanawake. Na kwa hili zimepokewa riwaya:

Hizi ninazokuletea ni zilizopokewa na masheikh wawili[3], kwamba Mtume (s.a.w.) amesema: "Mwenye kusimama katika mwezi wa Ramadhani - yaani kwa kutekeleza Sunna zake - huku akiwa na imani huku akitegemea kupata thawabu, basi hufutiwa madhambi yake yaliyotangulia." Naye alifariki dunia hali ikiwa hivyo hivyo tu, yaani kusimama usiku wa Ramadhani hakukubadilika kwa alivyokuwa akifanya kabla na baada ya kufa kwake. Kisha ikaendelea kuwa hivyo hivyo wakati wa ukhalifa wa Abu Bakr na katika sehemu ya ukhalifa wa Umar.

Ametaja Bukhari katika *Kitabu Tarawih* kutoka kwa Abdur-Rahman bin Abdul Qariy[4] amesema: "Nilitoka na Umar katika usiku wa Ramadhani kwenda msikitini, tukaona watu makundi wametawanyika mpaka alipo-sema: Akasema Umar, 'naona vizuri kama mngeliwakusanya watu wote hao nyuma ya msomaji mmoja ingelikuwa vizuri zaidi,' kisha akaazimia, akawakusanya kwa Ubayya bin kaab. (Akasema): "Kisha nikatoka naye usiku mwingine na watu wakiwa wanaswali nyuma ya msomaji mmoja. Umar akasema: 'Hii ni bid'a iliyo bora zaidi…'
Allama Qastalani amesema pale alipofikia kwenye kauli yake Umar, 'bid'a iliyo bora zaidi hii..' asema Qastalani: "Umar ameiita hivyo kwa sababu

[3] Rejea *Sahih Bukhari*, kitabu cha Swala ya Tarawehe: uk. 52 Sehemu ya pili. Na rejea *Sahih Muslim* mlango wa *Targhiib fii qiyami Ramadhan wahuwa tarawih*, kwenye kitabu cha swalaatul musafir waqasruha uk. 176 na iliyoko baada yake katika Juzuu yake ya pili.

[4] Ni nasaba ya huko Qara, na yeye ni Ibn Daysh bin Muljim bin Halib Al-Madani huyu alikuwa ni mfanyakazi wa Umar katika Baytul Maal (hazina) naye ni kiongozi wa Bani Zuhra. Amepokea kutoka kwa Umar na Abi Talha, na Abu Ayyub, na amepokea kutoka kwake mwanawe Muhammad, na Zahri na Yahya bin Jaada bin Hubayra, alikufa mwaka 80 akiwa na miaka 78, angalia kitabu, *Al-Istiiab*; Juz. 2. uk. 381, Darul Kutub al Alamiyyah.

Mtume (s.a.w.) hakuisunnisha iwe kwa jamaa, wala pia haikuwa enzi za Abu Bakr Siddiq, wala usiku wa mwanzo, wala idadi hii."[5]

Pia rejea katika *Tuhfatul Bari* na vinginevyo miongoni mwa sherhe za Bukhari[6]

Amesema mwanachuoni Abul Walid Muhammad bin Shahna baada ya kutaja kifo cha Umar katika matukio ya mwaka 23 katika historia yake - *Rawdhatul Manadhir* - "Yeye ndiye wa kwanza aliyezuia kuuza mama wa watoto, na aliyewakusanya watu katika takbira nne za Swala ya jeneza (ya kumswalia maiti). Na ni wa kwanza aliyewakusanya watu kuswalishwa na imamu katika Swala ya Tarawehe.

Alipotaja Suyuti katika *'Tarikhul-Khulafaa'* akinakili kutoka kwa Al-Askari[7], amesema: "Yeye ndiye wa kwanza kuitwa Amirul-Mu'minin, na wa kwanza aliyeweka kusimama usiku wa Ramadhani kwa Tarawehe, wa kwanza kuharamisha muta'a, na wa kwanza kukusanya watu kwa Swala ya jeneza ya takbira nne..."

Muhammad bin Saad amesema: Ambapo amemtarjumu Umar katika juzuu ya tatu katika '*Tabaqaat*': "Yeye ndiye wa mwanzo kuweka watu kusimama kwa Tarawehe katika mwezi wa Ramadhani mwaka wa kumi na nne. Na akawekea watu Madina wasomaji (waswalishaji) wawili; mmoja wa wanaume na mmoja wa wanawake.

Amesema Abdul Bari katika kumueleza Umar katika *Al-Istiab*: "Naye

5 *Irshadu Sari fi sharh sahih Bikhari* cha Qastalani Juz. 4 uk. 656 Kitabu cha tarawih Mlango wa Fadhl mana qaama Ramadhan

6 *Fat-hul Bari*, Juz. 4 uk. 219

7 Hasan bin Abdallah bin Sahl bin Said bin Yahya ana kun'ya ya Abu Hilal Lughawiy ana kitabu '*Awaail*' alichokitunga Jumatano, mwezi kumi wa Shaaban, mwaka 395. *Kashfu dh-Dhunnuun*, Juz. 1 uk. 199.

ndiye wa kwanza aliyeinawirisha Saumu ya Ramadhani kwa Swala ya kuombea.[8]

Amesema Said Abdul Husein Sharafud Din akitoa maoni yake juu ya wenye kuihalalisha Swala ya Tarawihi: "Ni kama kwamba hao -Mungu awasamehe na sisi - wameiokoa hekima kwa kuswali Tarawehe, Mwenyezi Mungu na Mtume walikuwa wameghafilika nayo."

Bali wao ndio wameghafilika zaidi na hekima ya Mwenyezi Mungu katika sharia na mipango yake. Bali kutowekwa jamaa katika Sunna za mwezi wa Ramadhani hio ni ili yule mwenye kuitekeleza awe yu pekee, usiku wa manane, nyumbani kwake akimsikitikia huzuni zake Mola wake. Na akinong'ona naye na yaliyo muhimu kwake, akitawasali na upana wa rehma Yake, akitarajia, akitegemea, akiogopa, akirejea na kutubia, akiukubali uungu wa Mola wake, akijilinda, huku akiwa hapati makimbilio ila kwa Mola Mtukufu na hakuna uokovu ila kutoka Kwake.

Kwa sababu hii ndipo Allah akaziacha Sunna ziwe huru bila ya kifungo cha Swala ya jamaa ili watu wapate nafasi ya kuwa pekee na Allah tu, na kuzielekeza nyoyo zao Kwake. Na kumchangamkia Mola wao kwa viungo vyao, akapunguza mwenye kupunguza na akazidisha mwenye kuzidisha kama ilivyokuja katika Hadith za bwana wa watu."[9]

Ama kuiswali jamaa basi hupunguza manufaa haya na hupunguza faida zake.

Naongeza juu ya haya kuwa kutoziswali Sunna jamaa huzipa nyumba fungu la baraka na utukufu kwa kuziswali humo, na pia hupata fungu la kujizoesha kupenda na kuwa na nishati nazo na hiyo ni mahali pa kielelezo katika amali za akina baba, kina mama, kina babu na kina bibi, na pia

8 *Al-Istiaab* Juz. 3 uk. 236

9 *An-Nass wa – ijtihaad* cha Sayyid Sharafud-Din uk. 214 na *Al-Mawrid* uk. 26 Swalatut Tarawih

inaleta athari ya kuwajenga watoto juu ya hilo ambayo inamea katika akili zao na nyoyo zao.

Abdallah bin Mas'ud alimuuliza Mtume (s.a.w.): "Lipi lililo bora zaidi, kuswali msikitini au kuswali nyumbani kwangu?" Mtume akajibu: "Je huoni nyumba yangu iko karibu zaidi? Mimi kuswali nyumbani kwangu ni bora zaidi kuliko msikitini, ila tu ikiwa Swala za faradhi." (Ameipokea Ahmad na Ibn Majah na Ibn Khuzaima katika *sahih* yake, kama ilivyo katika *Baabu targhiibi fii swalaatin nafilah* kutoka *Kitabut-Targhiibi wat-tarhiib* cha Imamu Zakiyyud-Din Abdul Adhim bin Abdil Qawiyy Al-Mundhiriy.**10**

Na imepokewa kutoka kwa Zaid bin Thabit, kwamba Mtume (s.a.w.) amesema: "Enyi watu! Swalini majumbani mwenu, kwani bora ya Swala kwa mtu ni ya nyumbani kwake, ila tu Swala ya faradhi." (Ameipokea Nasai na Ibn Khuzayma katika *Sahih* yake).

Na imepokewa kutoka kwa Anas bin Malik. Amesema Mtume (s.a.w): "Zikirimuni nyumba zenu kwa kuswali baadhi ya Swala zenu."**11**

Imepokewa kutoka kwa Jabir, amesema. Amesema Mtume (s.a.w): "Mtu atakapotimiza Swala yake msikitini, basi na ajaalie fungu katika nyumba yake kwani Mwenyezi Mungu ni mwenye kujalia kheri kutokana na Swala nyumbani kwake." (Ameipokea Muslim na Ibn Khuzayma katika *Sahih* yake kwa Isnad ya Abi Said.**12**

10 *At-Targhiib wat-tarhiib,* Juz. 1, uk. 279

11 *At-Targhiib wat-tarhiib,* Juz. 1, uk.280

12 *Musnad Shamiyyiina* Juz. 2, uk. 1021, *Muntakhab Musnad Abd bin Hamid*, uk. 3000 na uk. 969

Lakini khalifa ni mtu wa kuweka mpangilio ilimfungukia kuwa kuswali jamaa ni katika kuyafanya yatukuke mambo ya Mwenyezi Mungu, huku kukiwa na faida nyingi zisizo na idadi za kijamii, na wewe unafahamu kwamba Uislam haukupuuza upande huu bali ulihusisha Swala za wajib hapo na na kuziacha za Sunna upande mwingine wa maslahi ya[13] watu. Amesema Mwenyezi Mungu (s.w.t.): **"Na haiwi kwa muumini mwanamume au mwanamke, anapohukumu jambo Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wawe na khiyari….."**

Maoni ya Shi'a Imamiyya juu ya Swala ya Tarawehe

Shi'a Imamiyya - wakimfuata Mtume na Ahlul-Bait wake - wanazitekeleza Swala za Sunna za Ramadhani bila ya jamaa na wanaona kuwa kuziswali kwa jamaa ni *bid'a* isiyowekwa, isiyokubalika kisheria iliyozuka baada ya Mtume (s.a.w.) kwa kiasi na haikuteremka hoja kwazo ya Mwenyezi Mungu.

Sheikh Tusi amesema: "Sunna za Swala za Ramadhani huswaliwa na watu, mmoja mmoja, na kuswali jamaa ni *bid'a.*"

Ameitolea dalili madhehebu ya Imamiyya kuafikiana kwao kuwa hiyo ni *bid'a*, na alivyopokea Zaid bin Thabit[14] kwamba Mtume (s.a.w.) amesema: "Swala ya mtu nyumbani kwake ni bora zaidi kuliko kuswali msikitini, ila tu kwa Swala ya faradhi."[15]

13 **Ahzab: 36**
14 *Sunan Abu Daud*, Juz. 2, uk. 69
15 *Al-Khilaf*, Jz. 1, uk. 529 Kitabu cha Swala Mas-ala Na. 268

Na katika kitabu, '*Jawaahir*', kilichotungwa na Sheikh Muhammad Hasan Najafi amesema: "Kuwepo kwa uwezekano wa kiwango cha kuwa Hadith tawaatur juu ya *bid'a* ya kuswali jamaa katika Sunna za Ramadhani.[16]

Swala ya Tarawehe katika nass za Ahlul Bayt

Ama Maimamu wa Ahlul-bayt wameafikiana neno lao kwamba kuswali jamaa katika Swala za Sunna ni bid'a kabisa. Bila ya kutofautisha kati ya Swala ya tarawehe au nyingine kuna aina mbili ya riwaya zilizotoka kwao:
Zinazoonyesha si sheria jamaa katika Swala za Sunna.
Zinazooyesha si sheria jamaa katika Swala ya Tarawehe

Ama ya kwanza tunataja riwaya mbili:

Kwanza: Amesema Imam Baqir (a.s.): "Swala ya Sunna haiswaliwi jamaa, kwani hilo ni *bid'a*, na kila *bid'a* ni upotevu, na kila upotevu ni motoni."[17]

Pili: Amesema Imam Ali bin Musa Ridha (a.s.) katika barua yake kwa Ma'amun: "Haijuzu kuswaliwa jamaa katika Swala za Sunna kwani hilo ni bid'a."[18]

Ama aina ya pili ameizungumzia Imam Sadiq (a.s.) kasema: "Alipokwenda Amirul-Mu'minin al-Kufa, Hasan bin Ali (a.s.) aliamuru waitwe waambiwe watu kuwa hakuna Swala katika mwezi wa Ramadhani ya jamaa msikitini, Hasan bin Ali (a.s.) akanadi kwa watu alivyoamriwa na Amirul-Mu'minin (a.s.). Watu waliposikia aliyosema Hasan (a.s.) wakapiga mayowe: Ee Umar ee! Ee Umar Ee! Hasan aliporejea kwa Amirul-

16 *Jawahirul Kalaam*, Juz. 13, uk. 144

17 *Al-Khiswaal,* Juz. 2, uk. 152

18 *Uyuunul-Akhbar Ridha,* Juz. uk. 131

Mu'minin akamuuliza:" Ni sauti gani hizi?" Akajibu: "Ni watu, wanapiga mayowe Ee Umar! Ee Umar! Akasema Amirul-Mu'minin: "Waambie, swalini!."[19]

Pengine msomaji atastaajabu kwa kauli ya Imamu akisema: "Waambie, swalini." Ambapo aliwaacha wakiendelea kufanya jambo hili lililozushwa lakini akirejea katika maneno yake mengine inadhihirika kwake siri ya kuwaacha wao kuendelea vile walivyokuwa wakifanya.

Sheikh Tusi amesema: "Ama Amirul-Mu'minin alipokataza, alikataza kukusanyika, lakini hakukataza Swala yenyewe na alipoona kuwa jambo hilo linawafitinisha watu akajuzisha jambo lao la kuswali walivyozoea."[20]

Na inajulisha juu ya hilo alivyopokea Sulaym bin Qays, amesema: "Amirul-Mu'minin alihutubia akamhimidi Mwenyezi Mungu, akamswalia Mtume, kisha akasema: "Jambo ninalowahofia zaidi ni mambo mawili: Kufuata hawaa zenu na tamaa ndefu (kubwa)."

Kisha akataja yaliyotokea baada ya Mtume (s.a.w.) akasema: "Lau ningeliwaamrisha watu kuacha basi majeshi yangu yangelifarikiana mpaka nikabaki peke yangu au na wachache tu katika wafuasi wangu. Wallahi nimewaamrsiha watu wasikusanyike kwa jamaa katika mwezi wa Ramadhani ila kwa Swala ya faradhi tu. Na nikawajulisha kuwa kuswali jamaaa Swala za Sunna ni *bid'a,* baadhi ya wanajeshi waliokuwa nami wakanadi wakisea, enyi waislamu! Sunna ya Umar imebadilishwa, anatukataza kuswali huyu Sunna mwezi wa Ramadhani! Niliogopa kusitokee mapinduzi kutoka kwa baadhi ya jeshi langu."[21]

19 *Tahdhibul-Ahkam*, Juz.3 uk. 70

20 Rejea iliyopita

21 *Al-Kafi,* Juz. 8, uk. 63-85

Imam Ali alipata ukhalifa bila kulazimisha na kupenda kwa watu na alipambana na matukio baada ya kufariki Mtume (s.a.w.) na alitaka kuurejesha umma wa kiislamu kwenye ilivyokuwa wakati wa Mtume (s.a.w.) katika nyanja mbali mbali lakini kulikuwa na vikwazo, akaacha baadhi ya mambo vile yalivyo ili ashughulike na yaliyo ya muhimu zaidi ndipo alimuamuru mwanawe Hasan (a.s.) awaache watu walivyo ili usiharibike utaratibu wa mji na jeshi lisimgeukie.

Amepokea Abul Qasim bin Quwailiy (aliyefariki 369 A.H.) kutoka kwa maimamu wawili, Baqir na Sadiq (a.s.) kwamba wao wamesema: "Alikuwa Amirul-Mu'minin huko Kufa watu wanapomjia wakitaka awawekee Imamu wa Swala za Ramadhani huwaambia: "La." Na aliwakataza wasiswali jamaa mara wakaanza kulia kwa jina la Ramadhani, ee Ramadhani! Harith akaenda kwa watu akasema: "Ee Amirul-Mu'minin, watu wanapiga kelele na wamechukia ulivyosema. Amesema. Akasema Amirul-Mu'minin: "Waache wafanye wanavyotaka, waswalishwe na wanayemtaka."[22]

Riwaya hizi zinatufafanulia msimamo wa Ahlul-bayt juu ya Swala ya Tarawehe.

Sunna ya Mtume katika riwaya za Ahlul-Bayt

Riwaya za Ahlul-Bayt zinahitilafiana na baadhi ya riwaya za wenye *Sunnanu*. Kwa kuwa riwaya za Ahlul-Bayt ziko wazi kwamba Mtume (s.a.w.) alikuwa akikataza kuswaliwa jamaa Swala za Sunna za mwezi wa Ramadhani, na kwamba yeye Mtume alipotoka katika baadhi ya mikesha kwenda msikitini ili aswali peke yake watu walimfuata, aliwakataza hilo, na alipohisi kuwa wanasisitiza, aliacha kuswali msikitini na akawa akiziswali Sunna hizo nyumbani. Hizi hapa baadhi ya riwaya:

22 *As-Saraair,* Juz. 3, uk. 638

Zarara na Muhammad bin Muslim na Faidhwal waliwauliza Al-Baqir na Sadiq (a.s.) juu ya kuswali Sunna za mwezi wa Ramadhani kwa jamaa, wakasema: “Mtume (s.a.w.) alikuwa anapomaliza kuswali Swala ya Isha alikwenda nyumbani kwake, kisha huenda mwisho wa usiku msikitini na akaswali, akatoka katika mwanzo wa usiku wa Ramadhani ili aswali, watu wakapiga safu nyuma yake, akawakimbia na kwenda nyumbani kwake, akawaacha.

Wakafanya hivyo muda wa siku tatu, siku ya nne akasimama kwenye mimbari akamhimidi Mwenyezi Mungu kisha akasema: “Enyi watu! Hakika kuswali jamaa Sunna za usiku wa Ramadhani ni bid’a, na Swala ya Dhuha pia ni bid’a, tambueni! Msikusanyike kwa kuswali jamaa katika usiku wa Ramadhani wala msiswali Swala ya Dhuha, kwani hayo ni maasi, tambueni! Kila bid’a ni upotevu, na kila upotevu njia yake ni ya kuelekea motoni.” Kisha akateremka huku akisema: “Sunna iliyo chache ni bora kuliko bid’a iliyo nyingi.”[23]

Amepokea Ubaid bin Zurara, kutoka kwa Sadiq (a.s.) alisema: “Alikuwa Mtume (s.a.w.) akizidisha katika Swala yake katika mwezi wa Ramadhani, anaposwali usiku huswali baada yake; watu wakawa husimama nyuma yake, basi huingia na kuwaacha kisha hutoka, kisha huja tena wakasimama nyuma yake, yeye hutoka na kuingia mara nyingi.”[24]

Huenda Mtume alisimama kwa amali hii mara mbili, mara moja ni mwisho wa usiku - kama ilivyo katika riwaya iliyotangulia - na mara nyingine ni baada ya Swala ya usiku kama ilivyo katika riwaya ya pili.

23 *Man laa Yahdhuruhu*, Kitabus swawm, uk. 87

24 *Al-Kafi,* Juz. 4, uk. 154

Msimamo wa Sahih mbili juu ya Swala ya Tarawehi

Lakini yaliyopokewa kwa njia ya Sunni ni kinyume na hivyo. Hebu angalia nass za mashekhe wawili, Bukhari na Muslim:

Wa kwanza alipokea akasema: "amenihadithia Yahya bin Bakiir, ametuhadithia - Layth, kutoka kwa Aqil, kutoka kwa Shihab, ameniambia Urwa kwamba Aisha (r.a.) alimwambia kuwa Mtume (s.a.w.) alitoka usiku wa manane akaswali msikitini, watu wakaswali Swala yake, kulipokucha watu wakahadithia, wakakusanyika wengi wao zaidi, yeye akaswali na watu wakaswali naye, wakati kulipokucha watu wakazungumzia hilo, usiku wa tatu watu wakazidi kuwa wengi msikitini, katika usiku wa tatu, Mtume (s.a.w.) akatoka, akaswali Swala yake.

Ulipokuwa usiku wa nne, msikiti ulizidiwa na watu mpaka akatoka kuswali Swala ya Alfajr, alipomaliza, aliwaelekea watu akasema: "Nafasi yenu haikufichika mbali na mimi lakini mimi niliogopa isiwe ni faradhi kwenu msije mkashindwa nayo. Na Mtume alifariki hali ikiwa hivyo."[25]

Imepokewa pia katika mlango wa Tahajjud: "Kwamba Mtume (s.a.w.) usiku mmoja aliswali msikitini watu wakaswali naye Swala yake kisha akaswali usiku uliofuata, watu wakazidi wingi, kisha wakakusanyika usiku wa tatu au wa nne, hapo Mtume hakutoka kwenda msikitini, kulipokucha, akasema: "Nimeona mlivyofanya lakini hakuna lilionizuia kutoka kuja kwenu ila nilichelea isije ikawa ni faradhi kwenu na hiyo ni katika mwezi wa Ramadhani."[26]

25 Yaani ya kutoswali jamaa Swala ya Tarawehe, Angalia *Sahih Bukhari*

26 *Sahih Bukhari* Juz. 3, uk. 63 Babu Tahajjud bil layl na kati ya riwaya mbili hizi kuna hitilafu juu ya kutoka kwake, katika ya kwanza ni usiku wa tatu na nyingine masiku mawili.

Amepokea Muslim akasema: ‘Ametuhadithia Yahya bin Yahya akasema, “Nimesoma kwa Malik, kutoka kwa Shihab, kutoka kwa Urwa, kutoka kwa Aisha, kwamba Mtume (s.a.w.) usiku moja aliswali msikitini watu wakaswali naye Swala yake, kisha akaswali baadaye watu wakaswali naye pia, kwa wingi, kisha wakakusanyika katika usiku wa tatu au wa nne, [27] kisha hakutoka kuswali nao, kulipokucha, akasema: “Nimeona mlivyofanya, na hakuna lililonizia nisitoke ila niligopa isije ikawa ni faradhi kwenu, akasema, na hiyo ni katika mwezi wa Ramadhani.”

Na amenihadithia Harmala bin Yahya, ameniambia Abdallah bin Wahb, ameniambia Yunus bin Yazid, kutoka kwa Shihab, amesema: “Ameniambia Urwa bin Zubayr, kwamba Aisha alimwambia kuwa Mtume (s.a.w.) alitoka usiku wa manane akaswali msikitini, watu wakaswali naye, kulipokucha watu wakahadithia jambo hilo, wakakusanyika wengi zaidi katika wao, akatoka Mtume (s.a.w.) katika usiku wa pili pia wakaswali naye, asubuhi watu wakazungumzia hilo, usiku wa tatu watu wakawa wengi zaidi, akatoka, watu wakaswali naye, ulipokuwa usiku wa nne, msikiti ulishindwa kwa wingi wa watu, na Mtume hakutoka kuswali nao mpaka alipotoka tu wakati wa kuswali Swala ya Alfajr, akawaelekea watu, akasoma tashahud kisha akasema: “Mimi na jambo lenu la usiku huu lakini niliogopa isije ikafaradhishwa kwenu Swala ya usiku mkashindwa.”[28]

Tofauti ya walivyopokea watu wetu kutoka kwa Amirul-Mu’minin na walivyopokea masheikh wawili kwenye Sahih mbili ni wazi, ya kwanza ni jinsi Mtume alivyokataza kuswali Sunna hizo jamaa, na akaiita ni bid’a, na ya pili, Mtume mwenyewe aliacha kuswali jamaa kwa kuchelea isije ikafaradhishwa kwa watu, pamoja na kuwa inaafikiana na dini, na sharia. Kwa hivyo, ni ipi iliyo ya kweli kufuatwa?

27 *Sahih* Juz. 6, uk. 41 na nyingine

28 *Sahih Muslim*, Juz. 6, uk. 41

Mjadala kuhusu *Sahih* mbili

Katika Hadith za masheikh wawili kuna mushkili ambazo ni vizuri kuzielewa:
Mushkeli wa kwanza: Nini maana ya kauli, 'Nimeogopa msije mkafaradhishiwa kisha mkashindwa kutekeleza?'

Je maana yake: Kigezo cha kuweka sharia huwa ni watu kuifuata au kuiepuka! kama kuna hima iliyo dhahiri kwa watu watafaradhishiwa au sivyo hawafaradhishiwi? Hali ikiwa kigezo cha faradhi ni kuwepo kwa maslahi ya dhati katika hukmu, sawa kuwe kuna kutiliwa muhimu au la, kwani uwekaji sharia wa Mwenyezi Mungu haufuati kupenda watu au kutopenda kwao bali unafuata mkusanyiko wa maslahi na maovu ambayo Yeye anayajua zaidi, sawa iwe watu wamelifuata au wameliepuka.

Mushkeli wa pili: Lau tukichukulia kuwa maswahaba wameipa umuhimu Swala ya Tarawehe kuiswali jamaa, je hicho kitakuwa ndio kigezo cha kuwekwa faradhi? Msikiti wa Mtume wakati huo ulikuwa hauna nafasi kubwa hauchukui zaidi ya watu elfu sita, imekuja katika kitabu '*Fiqh ala Madhaahibil Khamsa*' kuwa: "Msikiti wa Mtume (s.a.w.) ulikuwa ni mita 35 kwa 30 kisha Mtume akaupanua na ukawa mita 57 kwa 50."[29]

Je inawezekana kufanywe kutilia umuhimu kwao kuwe kunafichua utiliaji muhimu wa watu wote katika zama zote hadi siku ya Kiyama?

Mushkeli wa tatu: Ni kuwepo tofauti ya idadi ya mikesha ambayo Mtume aliswali Sunna za mwezi wa Ramadhani jamaa.

Alivyopokea Bukhari katika kitabu cha Sawum ni kwamba Mtume (s.a.w.) aliswali Tarawehe na watu mikesha minne, na alivyonakili katika mlango wa Tahriidhu ala qiyamil'Layl, (kuhimiza Swala za usiku) ni kwamba

29 *Al-Fiqhu alaa Madhahibul-Khamsa* uk. 285

aliswali mikesha miwili, na Muslim akamuwafiki katika nukuu ya pili.

Na inadhihiri walivyonakili wengine ni kuwa Mtume aliswali katika mikesha tofauti, (usiku wa tano na wa tatu; Ishirini na saba) na hii inaonyesha kutokuwa na kutiliwa umuhimu kwa nukuu jinsi alivyofanya Mtume (s.a.w.) je tutakubali vipi katika nyingine zilizokuja kwamba Mtume alipendezewa na amali zao?

Mushkeli wa nne: Iliyothibiti katika amali ya Mtume ni kwamba aliswali mikesha miwili, au wa nne katika mwisho wa usiku, nazo hazizidi rakaa nane. Na ***Ta'asiy*** (kufuata) inabidi afuatwe Mtume katika ambalo limethibiti, lakini si katika lile lisilothibiti bali imethibiti kutokuwepo kama alivyoeleza kwa uwazi Qastalani, na kueleza kuwa iliokuwa zaidi ni bid'a. Na hivyo ni:
Mtume hakuwasunnia iwe ni Swala ya jamaa
Wala haikuwa enzi za Siddiq (Abu Bakr).
Wala usiku wa kwanza
Wala[30] si kila usiku

5. Wala si kwa idadi hii 30

Kisha alitegemea ijtihadi ya Khalifa kuthibitisha uhalali wake.

Amesema Al-Ayni kwamba: "Mtume (s.a.w.) hakuwawekea Sunna hiyo wala haikuwa wakati wa Abu Bakr, kisha Al-Ayni - katika uhalali wake alitegemea ijtihadi na istinbati ya Umar kutokana na taqriri kisheria kuwa watu - walikuwa - wanaswali nyuma yake mikesha miwili."[31]

Mushkel wa tano: Tukichukua riwaya ya 'kimoja cha vizito viwili,' (Ahlu Bayt), inakuwa kuswali Sunna jamaaa ni bid'a moja kwa moja,. tukichukua za mashekhe wawili, kiasi kilicho thibiti, ni kilichokuja kutoka

30 *Irshadu Saari,* Juz. 4 uk. 656 Kitabu Swalat Tarawih, Babu fadhl man qaama Ramadhaan

31 *Umdatul Qarii*, Juz. 6, uk. 126 Kitabu Tarawih Hadith Na. 116

maneno ya Qastalani, na zaidi inakuwa ni bid'a, makusudio ni amali yenyewe kwa dhati yake ni yenye kuwekwa, lakini namna inavyofanywa haikuwekwa kisheria.

Na hakikubaki kiwezacho kutolewa hodja kuhusu uhalali wake inyohitajiwa ila khalifa kukusanya watu nyuma ya imamu mmoja, nayo na hilo tutalifafanua katika utafiti ufuatao:

Kukusanya watu nyuma ya imamu mmoja wakati wa khalifa Umar

Amepokea Bukhari: Mtume (s.a.w.) alifariki na watu walikuwa juu ya hilo (la kuswali Tarawehe bila ya jamaa) kisha ikawa hivyo hivyo wakati wa Abu Bakr na mwanzoni mwa enzi za Umar.[32]

Imepokewa kutoka kwa Abdur-Rahman bin Abdul Qarii amesema: "Nilitoka na Umar bin Khattab usiku mmoja katika mwezi wa Ramadhani, kwenda msikitini, mara tukaona watu makundi wametawanyika, kila mtu anaswali peke yake, au mtu huswali Swala yake na kikundi cha watu.[33]

Umar akasema: "Mimi naona kama ningeliwakusanya hawa wawe nyuma ya msomaji (imamu) mmoja ingelikuwa ni bora zaidi, kisha akaazimia, akawakusanya nyuma ya Ubayy bin Ka'ab kisha nikatoka kwenda naye usiku mwingine, na watu wakiswali jamaa, Umar akasema: "Bid'a nzuri iliyoje hii, lakini ile ambayo wanaiacha kuiswali bali huwa wamelala katika muda wake ni bora kuliko hii wanayoiswali sasa. - yaani akikusudia mwisho wa usiku - na watu walikuwa wakisimama kuswali mwanzo wa usiku.
Lakini iliyo dhahiri kutoka kwa wafafanuzi wa Hadith ni kwamba kuswali

32 *Sahih*, mlango wa Man qaama Ramadhaan, Hadith Na. 2010

33 Baina ya watatu hadi kumi.

jamaa haikuwa imewekwa; na ubainifu wake wakujia ndani ya mambo mwili:

1. Kauli yake: "Alikufa Mtume (s.a.w.) na watu wakiwa hivyo, kisha jambo likawa hivyo enzi za ukhalifa wa Abu Bakr." Wafafanuzi wamesema kuwa, yaani hiyo ni kuwacha jamaa ya Tarawehe wala Mtume hakuwa amewakusanya watu kuswali jamaa."[34]

Badru-Din Al-Aini amesema: "Na watu wakiwa juu ya hilo, yaani la kuwacha kuswali jamaa. Kisha akasema: "Ukisema amepokea Wahb kutoka kwa Abu Huraira, alitoka Mtume na watu katika mwezi wa Ramadhani wanaswali upande wa msikiti, akasema: "Ni nini hii?" Akaambiwa: "Ni watu wanaoswalishwa na Ubayya bin Kaab." Akasema: "Wamepata, ni jambo zuri walilolifanya."

Ameitaja Ibn Abdul Barri. Kisha akaijibu kwa kauli yake: "Nimesema, Nilisema: ndani yake kuna Muslim bin Khalid naye ni dhaifu, iliyohifadhiwa ni kuwa Umar (r.a.) ndiye aliyewakusanya watu kuswalishwa na Ubayy bin Ka'ab."[35]

Qastalani amesema: "Na jambo lilikuwa hivyo (la kuwacha jamaa ya Tarawehe) kisha jambo likawa hivyo wakati wa ukhalifa wa Abu Bakar, mpaka mwisho wa aliyoyataja."[36]

Kauli yake: "Bid'a nzuri hii" katika yaliyowekwa na khalifa mwenyewe wala hayahusiani na sharia, wanavyuoni wengi wamefafanua hili.
Qastalan amesema: "Umar ameiita bid'a kwa sababu Mtume (s.a.w)

34 *Fat'hul-Bari* ya Ibn Hajar Al-Asqalani: Juz. 4, uk. 203

35 *Umdatul-Qari fii Sharh Sahih Bukhari* Juz. 6, uk. 125 imekuaja pia kwa maswali na majibu katika kitabu *Fat'hul Bari.*

36 *Irshadu Sari*, Juz. 4, uk. 656. Kitabu cha Swalatu Tarawih. Mlango wa fadhlu man qaam Ramadhan.

hakuwawekea hiyo, wala haikuwa wakati wa Abu Bakr Siddiq, wala mwazo wa usiku wala usiku wote, wala idai hii, na kusimama mwezi wa ramadhani si bid'a kwa sababu Mtume alisema: "Wafuataeni walio baada yangu Abu Bakr na Umar, wakiafikiana maswahaba na Umar juu ya hilo hapo neno la bid'a linaondoka."

Al-Aini amesema: "Ameiita bid'a kwa sababu Mtume (s.a.w) hakuwawekea sunna hiyo, wala haikuwa wakati wa Abu Bakr wala Mtume (s.a.w.) hakulipendelea. [37]

Imeafikiwa na wanavyuoni wa kisunni kwamba Umar ndiye wa kwanza aliyeweka hiyo jamaa na kwa kuongezea maana hiyo tunataja miongoni mwa kauli zao:

1. Amesema Ibn Saad katika maelezo juu ya Umar: "Yeye ndiye wa kwanza aliyeweka kusimama Ramadhani kwa Tarawehe, na kuwakusanya watu kwa hilo. Na kuandika kwenye miji na hiyo ni katika mwezi wa Ramadhani mwaka wa kumi na nne."[38]

Amesema Abdul Barri katika kumueleza Umar: "Yeye ndiye aliyeutia nuru mwezi wa Ramadhan kwa Swala ya ***Ish'fai*** (yaani Swala za rakaa mbili mbili).

Amesema Al-Walid bin Shahna alipotaja kifo cha Umar katika matukio ya mwaka 23 A.H. "Yeye ni wa kwanza aliyekataza kuuza mama wa watoto, na ni wa kwanza kukusanya watu kuswali nyuma ya imam waswali Tarawehe."[39]

Ikiwa Mtume (s.a.w.) hakuweka Sunna ya jamaa, bali ni Umar, je hiki ni kigezo cha kuwa sheria au ni cha bid'a ya hiyo jamaa? Pamoja na kuwa

37 *Umdatul Qarii*, Juz. 6, uk. 126

38 *Tabaqat al-Kubra*, Juz. 3, uk. 281

39 *Rawdhatul-Manadhir* kama katika *An-Nass wal Ijtihad* uk. 150

binadamu hata Mtume hana haki dhati yake ya kuweka Sunna na sharia ila yeye(s.a.w) ni mwenye kufikisha sharia kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na mwenye kupewa ijaza kufanya Sunna je itajuzu kwa asiyekuwa Mtume kufanya yasiojuzu kwa Mtume (s.a.w)?

Hakika wahyi unafikisha uwekwaji sharia kwa Mtume Mtukufu na yeye ndiye anayepewa wahyi, na alipokufa ulikatika wahyi, na mlango wa kuweka sheria ukafungwa, umma hauna kingine cha kufanya ila ijtihad tu katika kutoa mwangaza wa kitabu cha Qur'ani na Sunna. Si kuweka sharia au Sunna, na anayeona kuwa mwengine asiyekuwa Mungu ana haki ya kuweka sharia, maana yake ni kuwa wahyi haujakatika.

Amesema Ibn Athir katika *Nihaya*: "Na katika aina hii ni kauli ya Umar, "ni bid'a nzuri hii," lilivyokuwa miongoni mwa matendo ya kheri na laingia katika uwigo wa kusifiwa ameliita bid'a na amelisifu. Ila Mtume (s.a.w.) hakuiweka kwao bali aliiswali baadhi ya mikesha kisha akaiacha hakudumu na hakuwakusanya watu kwayo, wala haikuwa wakati wa Abu Bakr, ila Umar aliwakusanya watu na kuwasunnia, ndio akaiita bid'a nayo kwa hakika ni Sunna, kwa kauli yake Mtume (s.a.w): "Shikamaneni na Sunna zangu na Sunna za makhalifa waongofu baada yangu," na kauli yake (s.a.w.): "Wafuateni walio baada yangu, Abu Bakr na Umar."[40]

Kuweka sharia ni jambo maalum kwa Mwenyezi Mungu

Hakika hao wakubwa, pamoja na kukubali kwao kuwa Mtume (s.a.w.) hakuweka sunna ya kuswaliwa jamaa Swala hiyo, wametegemeza uhalali wa kuiswali jamaa tendo la khalifa na maana ya hiyo ni kwamba khalifa ana haki ya kuweka Sunna na sharia, na hii inapingana na kongamano la umma, kwani mwanaadamu yeyote hana haki kuingilia mambo ya sharia

40 *An-Nihaya*, Juz. 1, uk. 106, 107 Babu maa' daal

baada ya kuwa imekwishakamilika, kwa kauli yake Mwenyezi Mungu: **"Leo hii nimewakamilishia dini yenu, na nimetimiza neema yangu kwenu, na nimewaridhieni Uislamu kuwa ndio dini (yenu)."**[41]

Maneno yake yanapingana na Qur'ani na Sunna kwani kuweka sharia ni haki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, hakumwachia yeyote, na Mtume (s.a.w) ni mwenye kuifikisha.

Naongeza juu ya hayo kwa kusema kuwa, ikiwa khalifa alipata nuru ya kijani katika nyanja ya kuweka sharia na Suna, kwa nini isiwe hivyo kwa maswahaba wengine? Pamoja na kuwa wengine walikuwa ni wenye kusoma zaidi kuliko yeye, kama vile Ubayy bin Kaab, na mwenye kuzijua faradhi zaidi, kama Zaid bin Thabit, na aliyekuwa msomi na mwenye uhodari zaidi katika hukmu kuliko yeye, kama Ali bin Abi Talib (a.s)?

Kama wote wangekuwa na uwezo huo, basi ufisadi ungelienea na jambo la dini lingeenea kuwa ovyo, ingelikuwa ni kijisanamu tu kinachochezewa na mikono ya wasiokuwa ma'sum.

Ama kushikamana na Hadith mbili tulizozitaja - lau sanad zake zingeswihi, basi hazilengi kuwa wana haki ya kuweka sharia, bali zaonyesha ulazima wa kuwafuata wao, kwani wao wanategemea Sunna za Mtume Mtukufu (s.a.w.) sio kuwa wao wana haki ya kuweka.

Ndio, inadhihiri kwa alivyopokea Suyuti, kutoka kwa Umar bin Abdul Aziz ambaye alikuwa akiitakidi kuwa makhalifa walikuwa na haki ya kuweka sharia, akasema: "Amesema Hajib bin Khalifa, nilimuona Umar bin Abdul Aziz akihutubu naye ni khalifa, akasema katika khutba yake, 'Tambueni! Kile alichotusunnia Mtume wa Mwenyezi Mungu na masahaba wake wawili hicho ni dini, basi tukichukue, na kilichowekwa na wasiokuwa hao basi tunakikataa."[42] Nayo kama uionavyo.

41 **Al-Maida: 3**

42 *Tarikhul-Khulafaa*, uk. 241

Vyovyote itakavyokuwa, Mwenyezi Mungu hakuachia jambo la dini yake katika kuweka sharia kwa kupitia njia isiyokuwa wahyi, na katika hilo amesema Shawkani: "Ukweli ni kwamba, kauli ya swahaba si hoja, kwani Mwenyezi Mungu hakumtuma kwa dini hii ila Mtume wetu Muhammad (s.a.w.) nasi hatuna Mtume ila mmoja tu na maswahaba na walio baada yake wamekalifishwa kwa usawa kufuata sharia yake ya Qur'ani na Sunna, na atakayesema kwamba hoja ya dini ya Mungu inasimama na wasiokuwa wawili hao, huyo amesema jambo lisilo na uthibitisho katika dini ya Mwenyezi Mungu, na amethibitisha sharia ambayo Mungu hakuiamrisha.**43**

Naam amenakili Qastalani, kutoka kwa Ibn Tini na wengineo, kwamba Umar ametoa hilo kutoka kwa habari ya Mtume (s.a.w) kwa aliyeswali naye katika mikesha hiyo japo alichukia kwao hilo kwa kuogopa lisije likawa faradhi kwao, alipoondoka Mtume, ithibati ya kutofaradhiwa ilipatikana, Umar akalipa uzito - la kuswali jamaa kwa kuwa - katika kuswali - peke peke kuna mfarakano wa neno, kuwa na maneno tofauti, na kwamba kuwa pamoja katika jambo moja ni kuwa na nishati zaidi kwa waswaliihina wengi.**44**

Yazingatiwe aliyosema - Kwanza: alivyotaja mwisho wa maneno yake ili ahalalishe watu wawe nyuma ya imamu mmoja mahali pa maimamu wengi, ambapo mjadala ni juu ya asili ya kuiswali jamaa, iwe ni imamu mmoja au wengi.

Pili, ni maana ya maneno yake kuwa kuna hukmu ambazo hazikufanywa pale Mtume alipokuwa hai kwa kizuizi maalum, kama vile kuogopa kuwa faradhi, lakini watu mmoja mmoja katika umma wana wasaa wa kuweka sharia baada ya kufa kwa Mtume (s.a.w). Maana yake ni kufungua mlango wa kuweka sharia kwa umma mpaka siku ya Kiyama.

43 *Irshadul Uquul*, uk. 361 Darul Kutubil-Ilmiyyah

44 *Fat'hul Bari*, Juz. 4, uk. 204

Huu ni msiba hakuna baada yake msiba mwingine kama huu, na ni kucheza na dini, na ni kufungua njia ya kuing'oa.

Uongo ili kujiepusha na aibu ya bid'a

Kutokana na yote haya inadhihirika kuwa sifa ya bid'a imejikita katika Swala ya Tarawehe na hasa kwa kauli yake Umar bin Khattab: "Mimi naona lau hao wote wangelikusanyika nyuma ya msomaji (imamu) mmoja, ingelikuwa ni vizuri zaidi… hii ni bora ya bid'a."[45]

Lau kama hii si bid'a, licha ya neno lake 'Mimi naona' na neno lake, - waziwazi - 'hii ni bora ya bid'a,' ni bid'a ipi nyingine tena?!

Ikiwa aliyeizusha Tarawehi kwa mara ya kwanza, kwa mujibu wa kauli ya Ibn Abdul Barri katika *Al-Istiaab*, na Suyuti, katika *Tarikhul-Khulafaa* na Muhammad bin Shahna katika *Rawdhatul-Manadhir*, - kama ilivyotangulia awali - kuwa si mwana bid'a, basi ni nani atakuwa - mwana bid'a?

Kutoka hapa imedhihiri majaribio ya kuitoa Tarawehe nje ya uwigo wa bid'a na kuiingiza kwenye Sunna na kuyapa maneno ya Umar maelezo: 'Hii ni bid'a bora, japo namna yake inakhalifu ilivyo dhahiri, nasi tunataja jaribio hili:
Jaribio la Ibn Abil-Hadid Al-Mutazili, ambapo ametaja neno 'bid'a' lina maana mbili, ya kwanza ni yale yanayokhalifu Qur'ani na Sunna, mfano kufunga siku ya nahri na ayyamu tashriiq, japo ni kufunga lakini zimekatazwa.

Ni yale ambayo haikuja *nass* (dalili), na waislamu waliyafanya baada ya kufa Mtume (s.a.w.).
Ikiwa inakusudiwa Swala ya Tarawehe ni bid'a kwa maana ya kwanza

45 *Sahih Bukhari*, Juz. 3, uk. 252, *Al-Muwatta*, uk. 73, *Kanzul-Ummal*, Juz. 8, uk. 408.

hatuipokei kuwa ni bid'a kwa maelezo haya, na kauli ya Umar: "Kwa kweli ni bid'a", ni kauli mashuhuri iliyopokewa lakini aliikusudia bid'a kwa maana ya pili.[46]

Laiti kama amesema maneno haya na hakudhihirisha kuyaamini, kwani kwa maana ya kwanza si bid'a, kwani kukhalifu Qur'ani na Sunna hakuitwi bid'a kunaitwa ijtihad, kuikabili dalili, hivyo basi inabaki maana ya bid'a imefungika kwa maana ya pili ambayo aliisema, neno la Umar linafungamana nayo, kwani bid'a ni ile iliyozuka bila ya kuwa katika mfano uliopita na Tarawehe ni katika hiyo.

Na bid'a siyo ile iliyowekwa kwa mfano wa kukhalifu mfano uliopita mpaka isemwe kuwa ni bid'a hiyo ni yenye kukhalifu Qur'ani na Sunna.

Kisha akasema katika ukurasa wa pili: "Je si inajuzu kwa mwanaadamu kuzusha katika Swala za Sunna kwa njia maalum na idadi ya rakaa maalum na haiwi hiyo ni makruh au haram? Hiyo inaingia chini ya yaliyotajwa katika fadhila za Swala za Sunna. Na Tarawehe inajuzu na imesunniwa ambayo imeingia katika jumla ya ubora wa Swala ya jamaa."

Sijui ni katika madhehebu gani ya kifiqhi yametimu maneno haya, inavyojulikana kwa waislamu ni kuwa ibada za wajib na za Sunna hazina mabadiliko na ufahamu wa ibada ni kuwapo kwa amri ya kisharia.

Endapo amri ya kisharia ikithibiti kwa namna ya wajibu au Sunna lililoamriwa litakuwa ibada, vinginevyo hapana. Na amri ya kisharia ina nafasi katika asili ya ibada, katika namna na umbo lake.

Kwa maana ya kuwa ibada ni jambo linalo simama juu ya amri - katika asili yake namna na umbo.

46 *Sharh Nahjul-Balaghah,* Juz. 12, uk. 284

Kama ambavyo mwanaadamu hana haki ya kuweka asili ya ibada maalumu basi pia haifai kuweka namna ya kuifanya, pengine Ibn Abil-Hadid anaona kuwa amri ya Sunna, na yaliyokuja katika fadhila za jamaa yatosha kuthibiti uhalali wa Swala yenye namna iliyowekwa na mja, lakini kwa kweli haiko hivyo, Habari za fadhila za Sunna na Hadith zinazohusu fadhila za jamaa zinaashiria juu ya ibada zenye namna maalum zilizotoka kwa Mtume (s.a.w.) na kuwataka waumini kuzifanya kwa namna ilivyosunniwa na yeye (s.a.w.).

Dkt. Yusuf Al-Qardhawi anasema: Kuhusu suala la ibada kusimama juu ya – amri:

"Sheikhul-Islam Ibn Taymiyya amesema: "Kwa kweli matendo ya waja kati ya maneno na kivitendo yako aina mbili: Ibada zinazoiweka vyema dini yao na ada wanazozihitajia katika dunia yao kwa kuangalia asili ya sharia, tunajua kuwa ibada ambazo ameziwajibisha Mwenyezi Mungu au amezipenda haikuthibiti kuamrishwa kwake ila kwa sharia, na ama ada ambazo wamezizoea watu katika dunia yao katika wanayoyahitajia asili ni kutokatazwa, hakikatazwi ila alichokikataza Mwenyezi Mungu, kwani kuamrishwa na kukatazwa ni sharia za Mungu na ibada hapana budi iwe imeamriwa, na iliyothibiti kuwa haikuamriwa vipi itahukumiwa kuwa imekatazwa?

Na kwa ajili hii Ahmad na wengineo miongoni mwa mafaqihi wanahadithi wanasema: kuwa asili ya ibada ni kuwa zimeshawekwa hakuna kuwekwa ila kilichowekwa na Mwenyezi Mungu, vinginevyo tutaingia kwenye kauli yake Mwenyezi Mungu, katika *Suratush - Shura* Aya ya 21**[47]**

Amesema Abu Yusuf na Muhammad: "Haizidi katika Swala ya usiku rakaa mbili kwa salaam moja."**[48]**

47 Shuraa: 21

48 *Al-Halaal wal haraam*, uk. 36

Na amesema katika *Muhadhab*: “Na Sunna ni kutoa salaam kila rakaa mbili kwa ilivyopokewa kutoka kwa Ibn Umar kwamba Mtume (s.a.w.) amesema: “Swala ya usiku ni rakaa mbili mbili na ukiona Asubuhi imekaribia, basi Swali witri, moja.”

Na kukusanya rakaa kwa kutoa salaam kumejuzu kama ilivyopokewa na Aisha, kwamba Mtume (s.a.w) alikuwa akiswali rakaa kumi na tatu na akifanya witri ya hizo, kwa tano, anakaa rakaa ya mwisho na anatoa salam naye amefanya witri ya rakaa saba na tano na hapambanui kati ya hizo kwa kutoa salaam.”

Na akifanya Swala ya Sunna rakaa moja imejuzu pia kwa ilivyopokewa na Umar (r.a.) alipita msikitini akaswali rakaa moja, akafuatwa na mtu, akasema, “ewe Amirul-Mu’minin hakika mimi nimeswali rakaa moja.” Akasema: “Hakika hiyo ni Sunna kwa anayetaka atazidisha na anayetaka atapunguza.”

Imepokewa kwa Nawawi kwa kauli: “Katika madhehebu ya wanavyuoni juu ya hilo, tumetaja kwamba yajuzu kwetu kukusanya rakaa nyingi za Sunna. Na ni bora zaidi katika Swala ya usiku na mchana kutoa salaam kila rakaa mbili na kwa hili ndivyo alivyosema Malik na Ahmad na Daud na Ibn Mundhir.

Na imepokewa kutoka kwa Hasan Al-Basri na Said bin Jubair, akasema Abu Hanifa: “Kutoa salaam ni kwenye rakaa ya pili au ya nne kwenye Swala ya mchana, ni sawa katika fadhila, wala haizidi hiyo, na Swala ya usiku ni rakaa mbili au nne au sita au nane kwa kutoa salam, wala haizidi, na alikuwa Ibn Umar akiswali mchana rakaa nne.”

Itawezekana vipi tena mtu adai kuwa baada ya maneno yote haya na rai hizi, kwamba hakuna aliyesema kuwa ni makruh au haram [49]kuswali rakaa thalathini kwa kutoa salaam moja? Kama alivyosema Al-Mutazili kwa

49 *Al-Majmau min Sharhil Muhaddhab*, Juz. 4 uk. 49-51

kukata.

Amesema Sheikh Yusuf Al-Bahrani katika '*Hadaiqun-Nadhira*': "Hapana shaka kuwa swala ila mtu anayekalifishwa anapoitakidi kuwa kilichozidishwa juu ya dalili hizi zinavyoonyesha iwe ni idadi maalum au wakati maalum, au namna maalum, na mfano wake ambayo dalili ya kisharia haikutaja, huyo atakuwa amefanya haram na ibada zake zitakuwa ni bid'a."**50**

Na bid'a si kwa namna ya Swala bali kwa namna ya vile anavyoitakidi katika wakati huo na idadi na namna bila ya kutolea dalili hayo.

2. Kujaribu kwa Qadhi Abdul Jabbar Al-Mutazili katika kitabu chake *Al-Mughni* ambapo ameandika hivi juu ya Tarawehe: "Ikiwa hiyo ni mwito wa Swala na ni kuhimiza katika kuhifadhi Qur'ani basi ni kitu gani kinachomzuia mtu asifanye kwa njia ambayo ni yenye kusunniwa?"**51**

Maneno yake haya yanarejea kwenye natija kuwa ya maneno ya Ibn Abil-Hadid Al-Mutazili, hapo jibu ndilo lile lile, kwamba Swala ni ibada na ibada ni kusudio la kujikurubisha na Mwenyezi Mungu, nako hakutimii ila baada ya kuthibitika kuwepo kwa amri ya Mwenyezi Mungu, na Swala ya Tarawehe kwa ilivyo na namna yake inavyofanywa haikusimamia kwenye amri ya kisharia, na kwa hivyo hapo kuifanya kwa anuani kuwa hiyo ni ibada iliyowekwa ni haram na ni bid'a inayochukiza katika dini.

Kujaribu Ibn Taymiyya juu ya alivyozingatia alivyosema Umar bin Al-Khattab kuwa Tarawehe ni bid'a, hiyo ni kuita kilugha tu, na si kisharia, kwani waislamu waliswali Tarawehe wakati wa Mtume (s.a.w.) na kwamba Mtume (s.a.w.) alitoka nao kwenda kuswali katika usiku mmoja au miwili kisha akaacha kwa sababu aliyoitaja, nayo ni 'hakuna lililonizuia nisitoke kuja kuswali na nyinyi ila niliogopa isije ikafaradhiwa kwenu, basi

50 *Al-Hadaaiqun-Nadhira,* Juz. 6 uk. 80

51 *As-Shafi fil Imamiyya*: Sharif Murtadha, Juz. 4, uk. 217

swalini majumbani mwenu.'

Na hilo - maneno ni ya Ibn Taymiyya - kwamba muktadha wa kutoka, upo - na kwamba yeye lau si kuogopa kufaradhiwa basi angelitoka kwenda kuswali nao.

Ulipofika wakati wa Umar yeye aliwakusanya watu nyuma ya msomaji mmoja, ndipo kwa kuwa kwenye aina hii - ya kukusanyika nyuma ya Imam mmoja, ambapo hawakuwa wakifanya hivyo hapo kabla, ikaitwa bid'a kwa sababu katika lugha huitwa hivyo, hata kama haikuwa ni bid'a kisharia."[52]

Wala si muhimu kwetu kuita kwa Umar kuwe kwa kisharia au ni kwa kilugha, la muhimu kwetu ni kuwa, kule kukubali kwake kuwa ameongeza jambo ambalo hawakulijua waislamu hapo awali, na jambo alilioliongeza - kulingana na ibara ya Ibn Tayimiyya mwenyewe - ni kukusanyika msikitini nyuma ya imamu mmoja pamoja na kuwasha taa, na hilo la kuwasha taa si muhimu kwetu kwa kuwa haliko ndani ya ibada, lililo muhimu kwetu ni la kukusanyika watu nyuma ya imam, na huenda Ibn Taymiyya ametaja kuwasha taa ili kumzuga msomaji kwamba alilolisimamia khalifa ni jambo lisiloingia ndani ya kiini cha ibada, na kwamba kukusanyika watu msikitini nyuma ya imam hilo ni sawa na kuwasha taa. Kama ambavyo haichukuliwi kuwasha taa kuwa ni bid'a kwa kuwa haiingi katika kiini cha ibada, vile vile haichukuliwi kukusanyika katika Swala na kuitekeleza jamaa ni bid'a, inakuwa natija ya maneno yake ni: Kwamba Umar hakuzusha katika sharia bali alizusha katika mambo yaliyo nje ya Swala kama kuwasha taa, na huku ni kuufunika ukweli na kuhadaa.

Imedhihiri kutokana na jibu la jaribio lililopita hapo awali kwamba kutekeleza Swala kwa jamaa ni jambo lililo kiini cha ibada, na haiwezekani kwa mja kuliingilia, hapana budi kwake kufuata amri ya mwenye

52 *Iqtidhaau Siraatul-Mustaqiim*, uk. 276 - 277

kumuwekea sharia, kinyume na kuweka taa ambako kuko nje ya ufahamu wa ibada na kuanzisha kwake hilo hakuitwi bid'a.

Ama madai ya kwamba Mtume alikwenda kwenye Tarawehe usiku mmoja au mikesha miwili, kisha akaacha, imeshadhihiri hapo mwanzoni kuwa si sahihi, nayo inapingana na kauli ya Umar: "Hii ni bora ya bid'a." Hakika neno lake hili linaonyesha kutokuwapo Tarawehe hapo mwanzoni; na kuleta kitendo baada ya kukatika kwa muda kitendo hicho, kukianzisha hakuitwi bid'a.

4. Kujaribu kugawanya bid'a kwa mujibu wa hukmu tano. Nako ndiko kubaya zaidi na kuko mbali na roho ya sharia ya kiislamu nayo inaakisi fikra walizoishi nazo wenye jaribio hili kuielekea Swala ya Tarawehe na kukubali Umar bin Al-Khattab kwa kusema wazi kwamba hiyo ni bid'a. Wamesema: "Bid'a inagawanyika kwenye: Iliyoharamishwa, makruh, mubah, wajib na Sunna."[53]

Na jibu lililo wazi la kifupi juu ya kujaribu huku ni kuwa bid'a ina maana moja ya wazi nayo ni kuigiza jambo lisilo la dini, wameafikiana waislamu Sunni na Shia kwamba maana hii haikubali kuigawanya kwa maana ya hukmu tano. Wala kwa mujibu wa kuwa ni nzuri au mbaya.

Naam, lau ingelikuwa bid'a ina maana tofauti baisi tungeliweza kusawirisha katika kuigawanya, lakini ina mana moja tu nayo ni maana inayolaumiwa iliyotajwa kwenye Sunna, na ambayo alitahadharisha Mtume (s.a.w.) na kutoa kiaga juu yake, kwa adhabu kali, natamani lau wale wanaoigawanya kwa hukmu tano wangelitoa ushahidi wa maneno yao na Aya au Hadith ya Mtume kushuhudia ukweli wa maneno yao.

53 *Fat'hul Bari*, Sherhe ya *Sahih Bukhari*, Juz. 13, uk. 252 Kitabul-itiswam, mlango wa kitabu na Sunna kwenye hashia ya Hadith Na. 7277, *Jamiul-Usuul fi Ahadith Rasuul* cha Ibn Athir Juz. 1, uk. 280, *Kitabul itisaam bil kitaab wa sunna*, mlango wa kwanza dalilul hadith Na. 67

Lakini hawawezi kufanya hivyo si kwa sababu Qura'ni na Hadith ndivyo viwili pekee visivyo na ushahidi wa mgao huu, bali kwa sababu kiakili ugawanyaji uliotajwa ni muhali, kama ambavyo haiwezekani kuigawanya dhulma mbaya na nzuri pia huwezi kugawanya bid'a nyingine nzuri na nyingine mbaya, kwani bid'a ni tamko lenye maana ya kuzusha katika sharia, na kulinasibishia lisilo kuwa miongoni mwa sharia kuwa ni miongoni mwa sharia. Na maana hii inalazimiana na ubaya na kulaumiwa.

Haiwezekani kuepukika kwa hali yoyote ambapo inachukuliwa kugawanya huko kulikotajwa ni kuwezekana baina ya bid'a na uovu, na kuweza kupatikana bid'a nzuri, hii ndio mwanzo unaonyesha kuwa nadharia ya kugawanya inakuwa ni maana ya kilugha ya bid'a, nayo ndiyo iliyozusha katika mfano uliopita, kwa hivyo huyu aliyeizusha yawezekana awe ni mzuri au awe ni mbaya, na hii haina mjadala.

Nasi hatuko katika maana ya kilugha, bali maneno yote ni katika maana ya kisharia, kwa hiyo wao wanaangukia kwenye kufanya makosa makubwa wanapozungmzia juu ya bid'a kwa maana ya kisharia, kisha wanadai katika kuigawanya na hasa wanaigawanya lakini wakifuata maana ya kilugha.

Hitimisho

Swala ya Tarawehi haina msingi katika Kitabu na Sunna, na maiamau wa Ahlu bayt wamesisitiza kuwa ni katika bid'a ambazo hazikuwekwa na Mwenye sharia, Mwenye hekima, kama ambavyo haikuwa wakati wa Mtume (s.a.w.), wakati wa Abu Bakr na baadhi ya wakati wa Umar bin Al-Khattab bali ni bid'a iliyodhihiri kwa amri ya khalifa wa pili Umar bin Khattab, na kwamba kila majaribio ya kuitakasa isiwe na sifa ya bid'a ni majaribio yaliyofeli.

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka kumi na saba
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudhar
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu

27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillahi ni sehemu ya Qur'ani
45. Sauti ya uadilifu wa Binadamu
46. Kufungua Safarini.
47. Kusujudu juu ya udongo.
48. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Maulidi

BACK COVER

Swala ya Tarawehe, ni Sunna au bid'a?

Wajib, katika sharia ya kiislamu, ni yale yanayomlazimu mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, kuyafanya, kwa kuzingatia kuwa ni mambo ya faradhi ili kufikia ukamilifu utakikanao, kwa kuwa kutokamilisha kutekeleza wajib unaohitajika ni kutofikia daraja inayohitajika.

Na *Mustahabbu* na *Sunna*, ni yale mambo yanayomzidishia ukamilifu na kuwa karibu zaidi na Mwenyezi Mungu (s.w.t.) yule mu'min mwenye kulazimika na kutekeleza wajib.

Swala ya Tarawehe ni Swala ya sunna inayoswaliwa mwezi wa Ramadhani na wafuasi wa madhehebu ya Sunni. Madhebu ya Shi'a Ithanaasheri (na Baadhi ya Masunni) hawaiswali Swala hii, na wanasema kwamba ni *bida'a.* Kwa hiyo, kumekuwa na kushutumiana na kutoafikiana baina ya madhehebu hizi mbili juu ya suala hili. Je, upi ni ukweli?

Mwandishi wa kitabu hiki **Shaikh Abdul Karim Al Bahbahani** analijadili suala hili kwa upeo wake kwa kutumia Qur'an, Sunna, na hoja za kielimu pamoja na mantiki, na kumuacha msomaji aamue mwenyewe ukweli ni upi kati ya kuitekeleza Swala ya Tarawehe au kutoitekeleza, au iwapo ni bida'a ama sio bida'a.

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
P.O. Box 19701
Dar es Salaam, Tanzania
Simu:+255 22 2110640
Simu/Fax: +255 22 2127555
Email: alitrah@raha.com
Website: www.alitrah.org
Online: www.alitrah.info